# *Uungu Wa Yesu Kristo*

Ndugu Graham, asante. Habari za asubuhi, kila mtu, na Krismasi njema kwenu nyote. Tuna furaha sana kurudi tena asubuhi ya leo, hapa Maskanini, kuwa pamoja na kundi hili dogo la kupendeza.

2 Mimi na Ndugu Graham tulikuwa tukijadiliana mle ndani hivi punde, jambo hilo. Akasema, "Ndugu Bill, una lolote moyoni mwako asubuhi ya leo?"

3 Nikasema, "Kristo tu." Amina. Hamna lingine. Daima tunayo. Na kwa hivyo hilo ni jambo la kawaida kwetu, kwamba tunaye.

4 Nilifika nimechelewa jana, kutoka Dallas, ambako tulikuwa na. . .mmoja wa mikutano adhimu sana. Na jambo ambalo tumekuwa tukiliombea, sasa linakaribia kutukia. Tayari liko kwenye msimu sasa hivi, yaani, kwa ajili ya uamsho wa nchi nzima. Wahudumu wote, jana, ninii. . .ama siku chache zilizopita, ambao wamekuwa na mhudumu wa kiwango chochote ama ukubwa, au, ibada, tulikutana pamoja huko—huko Dallas kwa ajili ya mkutano huu. Na kulikuwako na wahudumu kumi na watano, kumi na wanane kule ambao—ambao wanayo huduma ambayo huwa na watu kati ya elfu tatu na elfu kumi na tano, labda elfu ishirini. Raymond T. Richey, kwa mfano, na Bosworth, na—na Oral Roberts, na Jackson, na jamaa hao wote kule.

5 Ndugu Jackson, hivi majuzi usiku, katika mkutano wake, alikuwa na watu mia tano waliompokea Roho Mtakatifu kwa wakati mmoja, kwa hiyo hilo ni zuri kabisa.

6 Basi sote tulikutana pamoja jana, hivi majuzi, kwenye makubaliano ya kazi ya huu mwaka, kwamba tunaamini kwamba Mungu yuko hapa kufanya kazi na uamsho, ulimwengu haujawahi kuuona awali. Ninaamini, marafiki, kwamba tu—tunaingia tu kwenye kitu cha ajabu. Nao wahudumu hawa ambao labda watakuwa na kila usiku katika msimu huu ujao wa kiangazi, Bwana akituruhusu, kila usiku itakuwa angalau popote kutoka. . .kutakuwako na mahema kumi na matano au kumi na sita makubwa yamepigwa, labda zaidi ya hayo, ambayo huenea hadi watu elfu nane na elfu kumi, kote Marekani, wakati ule ule.

7 Loo, hatuna budi kuwa na uamsho sasa. Tayari umeanza, mamia na mamia wanaupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, wakiingia katika Ufalme wa Mungu sasa. Si kitu ambacho hata tunatazamia, baadaye kidogo, lakini ta—ta—tayari kipo sasa. Mungu anafanya hivyo sasa.

8 [Ndugu Graham Snelling anamwuliza Ndugu Branham kuhusu maikrofoni—Mh.] Naam, bwana, mimi . . . Naam, Ndugu Graham. Hilo ndilo jambo ambalo mimi sikuzote . . . Nzuri. Vema, mnajua, mimi na Ndugu Graham tunafanya kazi pamoja vizuri sana; yeye ni mrefu sana na mimi ni mfupi sana. Kwa hiyo mimi . . . [Ndugu Snelling anasema, "Yeye huchuma tunda la chini, nami nachuma matunda yote yaliyo juu."] Wakati mwingine inanibidi kumfanya ayatikise yapate kuanguka . . . [Sehemu tupu kwenye kanda.] Asante, Ndugu Graham. Bado sijaupigia huo hesabu, huo moto. Tunautaka madhabahuni, sivyo? Amina. Mbona, wewe . . .

9 Hivi majuzi usiku mahali tulipokuwa tumeketi, msongamano wa maelfu mle ndani kabisa, na wote wakipiga makofi na kumsifu Mungu, tulikuwa tu na wakati mzuri sana, tulikuwa na Moto papo hapo madhabahuni wakati huo.

10 Nasi tuna furaha sana kutangaza uamsho wa majira haya yajayo ya kiangazi. Sasa niko kwenye . . .

11 Nitakuwa pamoja na kanisa hapa, pamoja na Ndugu Graham na ninyi nyote, kwa siku nane ama kumi zijazo, Nadhani, nijuavyo mimi, nami ninataka kuwa katika kila ibada niwezayo. Kisha mimi . . .

12 Tuondoke hapo, hadi Houston, Texas, kwenye uwanja mduara. Wanalo jengo zuri kubwa kule linaloenea watu elfu kumi na saba, nasi tunatarajia tu wakati mzuri sana.

13 Tulijaribu kuwa na . . . sisi sote kuwa na mstari wa maombi kule chini, lakini hatungeweza kufanya hivyo; mhudumu mmoja mahali pamoja, na mwingine pengine, katika mstari wa maombi. Lakini, jamani, haingefaulu hivyo, basi ikambidi Ndugu Jaggers aendelee tu.

14 Na, aisee, jambo lingine ninalotaka kutangaza. Ndugu Jaggers alisimama na kuchukua msimamo kama tuliochukua huko Calgary. Yeye . . . Wabaptisti wa Kimishenari na Wabaptisti wa Hiari Huru, na wengineo (mnajua, Texas imejaa Wabaptisti), walimtetea, lakini Wabaptisti wa kimsingi waliinuka wakaushambulia huo—huo mpango. Na, loo, jinsi walivyomkashifu gazetini na kila mahali. Vema, yeye, walimwandikia maswali ya Biblia, kwa hiyo akawajibu. Nao wakapata ninii . . . baada ya kuwa na thibitisho lao wenyewe, kisha lundo fulani la msimamo wa kisiasa, mbona, hawangeuweka kwenye gazeti. Kwa hiyo Ndugu Jaggers, tuliitisha mkutano huko, na wahudumu sabini na watano wa huo mji walioshiriki wakaja pamoja, tukachukua fotokopi yake na kusema, "Je, huu ni uhuru wa kusema? Je, huu ni uhuru wa kutoa habari?" Namna hiyo, kisha tukaituma. Ndipo gazeti hilo likapoteza wasomaji wake elfu kumi kesho yake asubuhi.

15 Ndipo wakaja, wakilia, wakipiga magoti, wakasema, "Tutalichapisha gazetini, bure, haitawabidi kutulipa hata peni moja."

16 Loo, ndugu, sikilizeni, enyi kanisa. Wakati mmoja tuliishi kando ya njia ya reli; hatuishi mle tena. Tunaishi kwenye Barabara Kuu ya Haleluya sasa. Naam, bwana. Tumefika mamilioni. Tulikuwa, kulikuwako na mamia machache tu, lakini tunafika mamilioni, mamilioni sasa. Na tukiwa tumeunganika pamoja, sisi ndio kanisa lenye nguvu zaidi, kwa idadi, lililoko Marekani; hiyo ni kweli, loo, nadhani, ulimwenguni. Mwaka jana, pekee, tulikuwa na waongofu milioni moja na laki tano. Wazieni hilo, waongofu milioni moja na laki tano, katika watu wa Injili yote, yaani, pamoja na maagizo ya jumla mwaka jana. Loo, tunapanda juu sasa.

17 Na magazeti haya madogo na kadhalika ambayo yamekuwa yakininii . . . hayangezungumza juu ya Wakatoliki, waliwaogopa. Mnaona, walihofu kufanya hivyo. Lakini idadi yetu inaelekea papo hapo juu sasa. Tunazo haki. Hebu tudai haki yetu tuliyopewa na Mungu. Hiyo ni kweli. Kwa hivyo tunasonga mbele mwaka huu, huku Mungu akiwa msaada wetu na ngao yetu, kusababisha ninii . . . kujaribu tuwezavyo kuwa na uamsho. Sasa mimi . . .

18 [Mtu fulani anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Loo, hapa juu? Ninyi nyote mtalazimika kuniambia wakati wa kumalizia. Huko juu, moja kwa moja huko juu. Vema. Ninaweza kutembea *hivi* na kuangalia nyuma.

19 Na kwa hiyo, vema, ni wangapi wanaojisikia vizuri kwa ajili ya Krismasi? Semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Loo, jamani, jamani! Angalieni! Huu ni wakati wa kushangilia, wakati ambapo sisi sote tunaweza kuja pamoja na kumwabudu Kristo.

20 Nami si—sina, sina ujumbe, hata kidogo. Niliifungua tu Biblia hapa alipokuwa akizungumza pale. Nikageuka hapa, nikasema, "Kuzaliwa kwa Kristo kuko wapi?" Karibu kila mtu anazungumza juu yake sasa. Basi itabidi nisome kwa muda kidogo kisha nipate kitu, kisha niendelee tu kuyumbayumba mpaka Roho wa Bwana achukue jambo fulani.

21 Sasa, kuanza, hebu tuanzie katika Luka, mlango wa kwanza wa Luka. Huo ni mwanzo wa ku—kuzaliwa kwake Kristo. Nasi tutasoma baadhi humu, ama tufundishe tu baadhi ya Neno kama tunaweza. Hatujui yale Bwana atakayotufanyia, lakini tunatumaini tu kwamba atatupa baraka kuu.

22 Aisee, nilisikia matangazo yako. Yalikuwa ni mazuri. Endelea tu, endelea, lihubiri Neno.

23 Nilikuwa tu nikimwambia Ndugu Graham, mle ndani, "Kama kuliwahi kuwa na wakati ambapo Wakristo wanahitajiana, ni sasa hivi, sasa hivi." Lolote mfanyalo, wekeni

kando kila kitu; maana ninaamini, kwa neema ya Mungu... Nitazungumza tu juu ya hilo, kidogo, katika dakika chache, jinsi ambavyo tu—tunahitajiana sasa hivi.

24 Kubwa...Ninaamini kuwa tunakabiliwa...Je, mnanisikiliza? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vema. Tunakabiliwa, sasa, tunatazama mchezo mkubwa zaidi wa kuigiza ambao umewahi kuwekwa katika historia yote ya binadamu, ukifanya kazi hapa mbele zetu, huu uwanja mkuu wa ulimwengu hapa, na mchezo wa kuigiza ambao Mungu ataigiza, sasa hivi, hiyo ni kusema, inashangaza sana, kutazama kote ulimwenguni na kuona jinsi hilo jambo linavyosonga mbele pamoja. Loo, ni jambo linalokaribia kutukia, rafiki. Hili ambalo tumelizungumzia na kunena juu yake, sasa hivi liko hapa. Tayari limeanza, kila mahali, linazuka.

25 Kuna picha nzuri sana ningependa kuwaonyesha asubuhi ya leo. Ninamwona mwana-kondoo nje kondeni, akila. Maskini jamaa huyo anashikwa na wasiwasi naye ananinii tu... anashangaa. Nikitazama kule kwenye matete papo hapo nyuma yake, namwona simba akinyemelea, kimya kabisa. Mnaona? Akiupigisha chini mkia wake, akiiandaa miguu yake apate kumrukia ghafla.

26 Hilo ni kanisa huko nje kondeni. Giza la ukomunisti linatanda kote ulimwenguni, likifunika kama kivuli kikuu.

27 Na hii ndiyo kanuni ya utofautishaji. Hebu chukua kitu kama kabla ya mapambazuko, sikuzote huwa giza zaidi kabla ya mapambazuko kwa sababu kunapambazuka, kukisukuma giza. Nayo ni kanuni ya utofautishaji, mnaona, huifanya iwe giza zaidi kabla ya mapambazuko.

28 Nasi tuko katika jambo lile lile sasa. Huwa giza mno tu kabla ya mapambazuko. Vile vivuli vikubwa vya giza vinasukuma ndani, ili kutimiza yule mtu wa dhambi. Je, mliona, katika wakati uu huu wa Krismasi, nchi zote za kikomunisti, badala ya kumtuma Kristo horini, walituma vitabu vidogo vya Stalin, wakiweka picha ya Stalin juu yake; yule mpingamizi, ajiinuaye nafsi yake juu ya kila kiitwacho Mungu, na kadhalika, akiingiza sehemu kubwa ya ulimwengu katika makucha yake. Na jambo lingine basi, ambalo, yote haya, hayo ni kuyatimiza Maandiko.

29 Na halafu, tena, nawatakeni muone jambo lingine, mojawapo ya yanayotimia. Watu hawa ambao ni baridi katika makanisa haya baridi, wanainuka dhidi ya hii Huduma. Nayo Biblia ilisema, "Wangekuwa na mfano wa utauwa, lakini wakikana Nguvu zake; hao nao mjiepushe nao." Na wanachukua msimamo wao.

30 Ukomunisti unachukua msimamo wake.

31 Mungu asifiwe, Roho Mtakatifu anachukua msimamo Wake. Naam. "Adui atakapokuja kama mafuriko, basi nitainua

bendera dhidi yake." Hiyo ni kweli. Nalo Kanisa limechukua msimamo Wake, ninamaanisha Kanisa la Roho Mtakatifu.

32 Sasa hayo ndiyo tu yanayonivutia, enyi marafiki, nami niko hapa. Huko nje, nitawaombea wagonjwa. Lakini hapa ndani ninavutiwa na jambo moja, na hilo ni Kanisa la Mungu lililozaliwa mara ya pili. Hiyo ni kweli. Hilo ndilo linalonivutia, kwa vyovyote vile. Sivutiwi na sheria ndogo, na mashemasi, na kadhalika, namna hiyo, ama taratibu za makanisa. Ninavutiwa na ubatizo wa Roho Mtakatifu juu ya Kanisa, kwa siku hizi tunazoishi. Hiyo ndiyo sehemu ya kimsingi, na hiyo ndiyo tunayotafuta.

Maombi mafupi tu sasa.

33 Baba wa Mbinguni, shuka chini, asubuhi ya leo, miongoni mwetu. Tujalie, Bwana, na Roho wa Mungu aiongoze ibada. Ibariki kazi hapa, Bwana. Mbariki ndugu yetu, Ndugu Graham. Mungu, mpe maneno ya hekima usiku wa leo, kwenye matangazo ya redio, jalia aweze ku—kuwatikisa watu kwa . . . kwa kuhubiriwa kwa Neno. Tujalie, Bwana. Jalia wenye dhambi walie, wapige magoti chumbani mwao na kuitoa mioyo yao kwa Kristo. Kukiweko na wasioamini wowote hapa asubuhi ya leo, ama yeyote ambaye hajamkubali Kristo, na waje, pia.

34 Na sasa anzisha uamsho mioyoni mwa watu, asubuhi ya leo, Bwana. Jalia huu uwe ni wakati wa kufanywa upya, wakati ambapo Roho atafanywa upya. Na, Ee Baba, tungeomba hivi. Njoo utushike mkono, kila mmoja wetu, ututembeze kwenye njia hii hapa. Tuonyeshe picha hii kuu ambayo imewekwa taratibu hapa, ukizifunua siri Zako kwa mioyo ya watakatifu asubuhi ya leo, ili tuweze kuona kile kilichoko tu hapa nje mbele yetu. Ndipo tunaposhuka basi, Bwana, katika silaha za Mungu, jalia twende kama askari hodari, kukabiliana na adui. Lakini tunawezaje kumkabili isipokuwa tunajua mbinu zake? Basi utusaidie asubuhi ya leo kuelewa, na utuonyeshe . . . mbele yake huko, kusudi tujue mahali pa kukutana naye. Kwa kuwa tunaomba haya katika Jina la Yesu. Amina.

35 Hebu, mlango wa pili, hebu tusome haya.

> *Ikawa* kwamba *siku zile amri ilitoka kwa Kaisari Augusto,* kwa *ulimwengu wote,* kwamba *watozwe kodi.*
>
> *(Na ushuru huu ulifanywa kwanza . . .* na *liwali wa Shamu.)*
>
> *Basi wote wakaenda kutozwa ushuru, kila mtu mjini kwao.*
>
> *Yusufu* naye aliondoka *Galilaya* mpaka *mji wa Nazareti, mpaka* Uyahudi, hata *mji wa Daudi, uitwao Bethlehemu; (kwa kuwa yeye ni wa mbari na nyumba ya Daudi:)*

*Ili aandikwe pamoja na Mariamu mkewe, ambaye amemposa, naye ana mimba.*

*Ikawa, kwamba, katika kukaa huko, siku zake* za kuzaa *zikatimia.*

*Akamzaa mwanawe, kifungua mimba, akamvika nguo za kitoto, akamlaza katika hori ya kulia ng'ombe; kwa sababu hapakuwa na nafasi kwa ajili* yake *katika nyumba ya wageni.*

36 Sasa kama msingi tu, kwa. . .mpaka tutakapofikia sehemu yake ambayo ningeitumia asubuhi ya leo. Na ninyi nyote jiachilieni tu mwe katika Roho wa Bwana.

37 Sisi, leo, duniani kote, tunasherehekea kuzaliwa kwa Yesu, ambako sasa ni mapokeo tu. Yesu hakuzaliwa mnamo Desemba tano wala kitu kama hicho. . .au Desemba 25. Tunajua hilo haliwezekani. Milima ya Uyahudi ilikuwa imejaa theluji wakati huo, kwa hivyo hiyo ingewezekanaje? Yesu kwa kawaida, kwa unajimu, kadhalika, na kwa yote hayo alizaliwa, kwanza, kama tarehe moja Aprili, wakati ilipokuwa ni majira ya Kuchipusha. Lakini hii ni siku, ambayo ni sawa, iliyotengwa tu kuabudia, katika ukumbusho wa kuja Kwake ulimwenguni.

38 Mojawapo ya zawadi kuu zaidi ambazo Mungu amewahi kutoa kwa ulimwengu ilikuwa ni Yesu Kristo. Hilo, tunajua hilo. Na sasa nataka kunena, asubuhi ya leo, juu ya Uungu Wake, kwamba Yeye ni Nani. Wengi sana wanamdhania ni mtoto mchanga amelazwa pale kitandani, na kadhalika. Lakini hiyo—hiyo ilikuwa tu ni moja ya picha, moja tu ya maandalizi ya mchezo wa kuigiza, kuileta kufikia jinsi Yeye alivyo kweli, Uungu Wake.

39 Naye alisema, katika Maandiko ya kuja Kwake, Yeye angenenwa tangu siku za—za Yohana. Moja kwa moja hata kufikia Mwanzo, ilitabiriwa, ya kwamba, "Uzao wa mwanamke ungekiponda kichwa cha nyoka," likiahidi Mtoto—Mtoto huyu, Kristo Yesu. Naye amekuwa huko chini, manabii wote; karibu kila nabii aliyepata kuandikwa katika Biblia, alizungumza juu ya kuja Kwake mara ya kwanza na ya pili, wakati Yeye angekuja ulimwenguni.

40 Yesu anakuja mara tatu. Alikuja, mara ya kwanza, *kulikomboa* Kanisa Lake. Anakuja, mara ya pili, *kulipokea* Kanisa Lake. Anakuja, mara ya tatu, *pamoja na* Kanisa Lake. Kila kitu katika Biblia husafiri katika utatu, tatu-tatu, lakini wote katika Kristo mmoja. Yeye, kumbukeni, mara ya kwanza, *kulikomboa* Kanisa Lake; mara ya pili, *kupokea* Kanisa Lake; mara ya tatu, *pamoja na* Kanisa Lake, kama Mfalme na Malkia.

41 Sasa, lakini kwenye kuja Kwake mara ya kwanza, tutakuzungumzia kidogo tu, halafu juu ya kuwa Kwake hapa; halafu kwenye kuja Kwake mara ya pili, huko, juu yake; na kisha mara ya tatu; Bwana akipenda.

42 Sasa katika siku hizi, kulikuwa na mateso makubwa dhidi ya kanisa. Kaisari Agusto alikuwa amefanya mpango mkubwa, kwamba atawatoza watu wote ushuru. Na hilo lilifanyika kwa kusudi moja tu, kwamba unabii mkuu wa Mungu ungetimizwa.

43 Jambo pekee unalopaswa kufanya, unapoona jambo fulani katika Biblia, ambalo linasikika kidogo kuwa ni jambo la kubuni na la ushirikina kidogo kwako, mpe Mungu muda kidogo tu. Mungu hana haraka. Sisi ndio tunakuwa na haraka. Mpe Mungu muda kidogo tu, nawe utaona yale magurudumu ya kale ya kinabii, meno ya magurudumu, yakiingia moja kwa moja kwenye picha. Itasafishika, kama vile tu kuileta picha.

44 Kama vile mtu fulani alivyokuwa akizungumza hivi majuzi, akasema, "Mungu, Yeye alikuwa nini?" Alipokuwa huko nyuma, mamilioni na mamilioni ya miaka iliyopita, wakati Yeye hakuwa. . .kama tu uwazi huu hapa; na kisha akajikusanya katika Logos; halafu akatoka kwa Logos, akaja ndani ya Kristo. Mnaona, ni Mungu tu akishuka namna *hii*, duniani, kisha anarudi moja kwa moja kuwa Mungu tena. Hivi hamwoni ninalomaanisha? Akizunguka tu, akishuka kutoka angani, kutoka Umilele; akifingirika pamoja, akishuka akaingia katika Logos; kutoka kwa Logos, hapo akaingia ndani ya Mwanadamu, kisha anarudi moja kwa moja tena. Kwa kusudi moja, kumkomboa mtu yule aliyeanguka.

45 Sasa, hilo ndilo lililomleta, apate kuwa Mkombozi. Na kabla Mungu hajawa Mkombozi, ilimbidi awe, kulingana na sheria, Mkombozi wa jamaa. Ilibidi awe wa jamaa yetu.

46 Na Mungu hapo mwanzo alimwumba mtu wake wa kwanza, alimwumba kutoka katika roho. Nayo roho ni sehemu isiyoonekana ya mwanadamu, usiyoiona. Sasa Mungu alimwumba mtu kwa mfano Wake Mwenyewe. Je, mnanisikiliza? Vema. Mungu alimwumba mtu kwa mfano Wake Mwenyewe. "Naye Mungu ni Roho," ilisema Biblia. Naye mtu wa kwanza aliyeumbwa alikuwa na mamlaka juu ya viumbe vyote, kama vile tu Roho Mtakatifu alivyo na mamlaka juu ya Kanisa siku hizi. Aliongoza maumbile. Aliwaongoza wanyama.

47 Lakini hapakuwapo na mtu wa kuilima ardhi, kwa hiyo Mungu akamfanya mtu kutoka katika mavumbi ya ardhi. Na mtu huyo, huenda alimpa mikono kama tumbili, huenda alimpa miguu kama ya dubu. Chochote alichofanya, alivitupa pamoja tu na kumfanya mtu. Lakini mtu huyu, aliweka roho hii isiyopatikana na mauti, ambayo haifi kamwe, ndani ya mtu huyu, naye akawa zaidi ya mnyama; akawa mtu.

48 Kisha mtu huyu hapa, hivyo ndivyo ninavyowazia ambapo makafiri na baadhi yao wamesimama huku, wakibishana. Lakini saa imewadia ambapo Mungu ametoa Nuru Yake, hii hapa saa ambayo Mungu anafanya mambo. Hiyo ni kweli. Na kwa hivyo sasa wanapobishana, "Vema, miguu yake inaonekana

kama dubu, na mikono yake inaonekana kama nya—nyani au tu—tumbili, au kadhalika," na wanajaribu kusema asili yake imekuja huko. Hilo halina uhusiano wowote nalo.

49 Huu ndio mwili wa nyama ambao anaishi tu ndani yake, kama nyumba, unarudi kwenye mavumbi ya ardhi. Lakini ile roho haipatikani na mauti; inatoka kwa Mungu. Hiyo ndiyo sura ya Mungu. Mungu ni Roho.

50 Mtu huyo alipoteza asili yake katika bustani ya Edeni. Uhusiano wake, ushirika pamoja na Mungu ulikatizwa pale, kwa sababu ya dhambi na kutokuamini. Kutokuamini nini? Neno la Mungu. Wakati mmoja Hawa alichorewa picha, naye akaambiwa jinsi kungekuwa kwangavu zaidi kama tu yeye ange—angeachana tu na Neno la Mungu, "angalia hapa utoe hoja." Huwezi. Mungu . . .

51 Kuna tofauti kati ya hoja na Neno la Mungu. Neno la Mungu ni kweli; hoja ni ya uongo. Huwezi kutolea hoja chochote. Hiyo ni kweli. Akili zetu si nzuri, mnaona, si nzuri vya kutosha au kamwe hazitakuwa nzuri, kuifahamu hekima ya Milele ya Mungu. Na, kwa hiyo, huwezi kulitolea hoja; inakubidi tu kuliamini.

52 Na kwa hiyo basi hiyo picha ilichorwa, kule nyuma kupitia kwa baba na mama zetu wa kwanza, nao wakaanguka. Ndipo hilo likavunja uhusiano na Mungu, nao wakafukuzwa kutoka katika bustani ya Edeni. Tangu saa hiyo, Mungu akaanza kupiga mayowe huku na huku bustanini, akimtafuta mtoto Wa—Wake aliyepotea.

53 Ndipo basi njia pekee ambayo Mungu angeweza kumkomboa, ingembidi kufanya . . . kushuka na kumkomboa, Mwenyewe; si katika mwingine, si kumtuma mtu mwingine. Asingeweza kumtuma Malaika; hiyo isingekuwa sawa. Lakini njia pekee ambayo Mungu angeweza kumkomboa mtu huyo, ilikuwa ni kushuka Mwenyewe apate kumkomboa.

54 Mtu akitenda dhambi hapa, na, jamani, nilikuwa hakimu wa hili, wa kundi hili la watu, nami nilikuwa na mamlaka juu yenu nyote, na kama mimi . . . Kama mtu fulani alitenda dhambi, nami nikasema, "Sasa, mimi . . . Ndugu Graham, nataka wewe ulipie hiyo gharama." Hiyo haitakuwa haki. Kama nilisema mvulana wangu mwenyewe alipie hiyo gharama, hiyo bado haingekuwa . . . ? . . . haki. Njia pekee ambayo ningeweza kuwa mwenye haki, ni mimi mwenyewe kupachukua mahali pake. Na nini? Mimi ndiye niliyetoa hiyo hukumu, ndipo basi kama ninataka kumkomboa huyo mtu, sina budi kupachukua mahali pake, mimi mwenyewe. Mngali mnanisikiliza? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

55 Sasa, angalieni, ninataka muone jambo fulani. Ndipo wakati hii, njia pekee ambayo Mungu Mwenyewe angeweza kumkomboa mtu huyu, ilikuwa ni kushuka na kupachukua

mahali pake. Na hiyo ilikuwa ni sheria iliyotolewa na Musa, ya ukombozi, kwamba ilibidi iwe kupitia kwa mkombozi wa jamaa; kwanza mtu aliyestahili, mtu aliyestahili hiyo gharama, mtu ambaye angetoa ushuhuda wake hadharani na kukomboa mali iliyopotea ya mtu aliyeanguka. Na, basi, Mungu alikuwa mstahilifu. Alishuka yapata miaka elfu moja na mia tisa iliyopita, katika umbo la mtoto mchanga, aliyezaliwa horini, akafunikwa na Roho Mtakatifu, hakuzaliwa kwa kujuana kimwili. Alikuwa Mungu. Damu ya Mungu ilikuwa ndani Yake.

56 Mtoto sikuzote ni damu ya baba yake, sio ya mama yake. Sote tunajua hilo. Bila. . . Nimefundisha hayo awali, hapa, katika nyakati, nanyi mnajua kwamba mtoto hana chembe moja ya damu ya mama yake ndani yake, hata kidogo.

57 Hapana, hana kabisa. Daima ni damu ya huyo mwanamume. Kuku anaweza kutaga yai, lakini kama halikurutubishwa, kamwe halitaanguliwa. Haijalishi jinsi hilo yai lilivyo maridadi, na jinsi anavyolipasha joto vizuri, sikuzote litakuwa lisilorutubiwa. Litakaa papo hapo na kuoza, hiyo ni kweli, isipokuwa ndege dume amekuwa na ndege jike, nayo chembechembe ya uhai hutoka kwa dume.

58 Kwa hiyo, wakati Mariamu, "pasipo kumjua mwanaume," alikuwa pamoja na Mwanaume, Mungu, Yehova Mwenyezi, Naye akamtia uvuli, naye Mungu ndiye Muumba aliyeumba chembechembe ya Damu katika tumbo la uzazi la Mariamu, "pasipo kumjua mwanamume hata kidogo." Nayo hiyo ikaleta ile Damu umbivu yenyewe ya Mungu, apate kutukomboa kutoka kwenye maisha yetu ya kuja hapa kwa kuzaliwa na tamaa ya kujuana kimwili.

59 Halafu hiyo Damu ikatolewa katika mishipa ya Imanueli, juu ya msalaba wa Kalvari, na leo ina nguvu zile zile za kuokoa, za kukomboa, na takatifu kama ilivyokuwa siku ile ya kuongezewa damu mishipani ilipofanywa pale Kalvari. Mnaliamini? Amina! Sasa, hiyo ni kweli, tumekombolewa kwa Damu ya Mungu. Biblia inasema, "Tumenunuliwa kwa Damu, na kukombolewa kwa Damu, Damu ya Mungu Mwenyewe."

60 Ilikuwaje Damu ya Mungu? Mungu hana damu. Ingewezekanaje? Kwa sababu ilikuwa ni Damu umbaji ya Mungu aliyoiumba, apate kutukomboa, kisha akaja na kuishi katika mwili ule ule aliouumba. Kwa hiyo asingeweza. . . Ilimbidi Mungu kupitia majaribu; asingeweza kujaribiwa. Ilibidi apitie majaribu ya kujuana kimwili. Ilibidi apitie majaribu ya kila namna, kujaribiwa na ibilisi, katika utajiri na uweza na—na milki, na kadhalika. Ilibidi ateseke na yote hayo. Ili kufanya hivyo, asingeweza kuwa kama Mungu katika Roho; ilimbidi awe Mungu katika mwili.

61 Sasa ninazungumza asubuhi ya leo juu ya Uungu wa Kristo, ili kwamba mjue Yeye ni Nani tunayemwabudu siku

hizi. Sio mtoto mchanga horini, au si Baba Krismasi, lakini tunamwabudu Mungu Mwenyezi, katika Uungu wa Mwanawe.

62 Basi angalieni basi, hiyo Damu ilishuka na ikawa. . .nayo ilikuwa ni Kristo Yesu. Naye Mungu Mwenyewe, akitoka katika Roho, aliingia ndani ya Kristo Yesu. Nayo Biblia ilisema, ya kwamba, "Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake." Je, hiyo ni kweli? Mungu Mwenyewe, Yehova, aliishi ndani ya Kristo na akafanywa kuwa Jamaa yetu wa karibu, kwa sababu alizaliwa katika mwili wa mwanadamu kama sisi. Je, hiyo ni kweli? Seli za Damu zilibuniwa na Mungu, na—nazo chembe za nyama zilikuzwa katika tumbo la uzazi la Mariamu, ambalo lilimzaa yule Mtoto. Basi Mungu akashuka na kuishi katika mwili wa mwanadamu, na akajaribiwa kwa kila njia kama tunavyojaribiwa. Je, mnaamini hilo? Vema.

63 Sasa, basi, alipofanya jambo hilo, Yeye alitoa Damu Yake bure. Haikumbidi kufanya hivyo. Alitoa dhabihu hiyo. Angeweza kwenda moja kwa moja Utukufuni. Angeweza kugeuzwa sura kama vile alivyogeuzwa kwenye Mlima wa Kugeuka sura, aende zake Mbinguni na kamwe asife kwa ajili yetu. Lakini akiwa tayari kutufia sisi, alitoa Damu Yake bure pale Kalvari. Hiyo ni kweli. Naye akachagua. . .Alikuwa ni Mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitiko, Naye akatoa ushuhuda hadharani.

64 Katika Ru-. . .Kitabu cha Ruthu, ni picha nzuri sana pale, jinsi huyo Boazi, mfano wa Kristo, jinsi Ruthu alivyokwenda katika nchi ya kigeni, kama mtu aliyerudi nyuma, akatoka humo nchini, naye akaleta pamoja naye. . .Namaanisha Naomi, naye akamleta Ruthu aliporudi. Ndipo Ruthu aliporudi, alikuwa ninii. . .na wa nchi ya Moabu. Ndipo aliporudi, alikuwa Mmoabu; picha kabisa ya Bibi-arusi wa Mataifa, wa Kanisa.

65 Naye alipokwenda kumwacha Naomi, Naomi alimwambia, akasema. . .akambusu na kumwambia arudi kwa watu wake. Akasema, "Nitakwenda pamoja nawe kwa watu wako. Watu wako na wawe watu wangu, na makazi yako yawe makazi yangu, Mungu wako awe Mungu wangu, wala hakuna kitu ila mauti kitakachotutenganisha. Pale utakapofia, nitakufa nami. Utakapozikwa, nitazikwa."

66 Sasa hiyo hapo picha ya Kanisa la Mataifa likimjia Kristo. Maana, wakati mmoja tulikuwa wageni tuliomwacha Mungu, Wayahudi pekee ndio walikuwa—walikuwa waokolewe. Lakini sisi, tukiwa wafu katika Kristo, tunautwaa Uzao wa Ibrahimu, nasi tu warithi sawasawa na ahadi, naye Kristo akamchukua Bibi-arusi Mmataifa. Hiyo ni kweli kabisa.

67 Sasa ili kumkomboa, Boazi, kuikomboa mali ya Naomi iliyopotea (Hiyo ilikuwa ni hali ya kurudi nyuma ya Israeli.), kisha Moabu—Moabu ilimbidi atoke, na alipotoka, Boazi, hasa,

basi wakati alipotoka nje, ilimbidi avue kiatu chake mbele ya malango, mbele ya wazee, kutoa ushuhuda hadharani kwamba alikuwa amemkomboa mwanamke yule aliyepotea katika mali yake. Na katika kufanya hivyo, ndipo akanunua tena, pia, mle ndani akampata bibi-arusi wake, mwanamke a—aliyekuwa akimtafuta. Ilimbidi kumkomboa huyo mwanamke kwanza, ili ampate huyu bibi-arusi. Hivi hamwoni?

68 Na hilo ndilo jambo lile lile alilofanya Kristo. Alifanya ushuhuda wa hadharani kwenye malango ya Yerusalemu, wakati alipopigwa, akachapwa, akateswa, na kuongozwa pale juu Kalvari, kwenye Kal-. . .mlima wa Golgotha. Ndipo akakilowesha hicho kilima kwa Damu Yake Mwenyewe, kama ushuhuda wa hadharani ya kwamba alikuwa ameikomboa mali yote iliyoanguka tangu hapo mwanzo, na amewakomboa watu Wake kutoka katika laana ya dhambi na kutoka katika makucha ya Kuzimu.

69 Huku akijua ya kwamba angehitaji kitu cha zaidi katika siku za mwisho, kuliko kile alicho nacho sasa, Alisema, "Sitawaacha ukiwa. Nitamwomba Baba Naye atawapa mfariji mwingine, ambaye ni Roho Mtakatifu. Atakaa nanyi milele. Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena; lakini ninapanda juu Mbinguni na kukitayarisha kitu hiki, nami nitarudi na kuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari." Hicho ndicho ninachozungumzia. Mngali mnanisikia? Semeni, "Amina." Hiyo ni sawa. Hilo ndilo ninalozungumzia sasa, ni Yeye akija tena katika nguvu Zake.

70 Nyakati zimepita upesi, "Loo, Yeye ni Nani?" Jamani, asubuhi ya leo, wanawazia juu ya kitu kidogo cha kuabudiwa, maskini hori ndogo huko nje, ninii kidogo . . . Hiyo, siliwazii hilo.

71 Ninawazia juu ya Kristo, tumaini la Utukufu, mioyoni mwetu asubuhi ya leo, kwa Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli.

72 Loo, kuhukumiwa na ulimwengu! Mungu sikuzote amekuja ulimwenguni; alipokuja, ulimwengu ulimchukia. "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Mungu." Tuko katika siku hiyo, enyi marafiki.

73 Na sasa angalieni, "Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena; hata hivyo ninyi mtaniona Mimi, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari." Hiyo ni kweli. Yuko hapa sasa. "Na katika siku . . . " Jinsi picha Yake kubwa ilivyozunguka sikuzote na kufanya jambo lile lile ambalo tunaliona sasa. Mchezo mkuu wa kuigiza umetayarishwa, nasi tuko tayari sasa kuona mambo makubwa yakitokea.

74 Kanisa limetolewa utotoni. Hiyo ni kweli. Pentekoste ililipembeza kule chini, miaka michache iliyopita, huko nyuma wakati watu wakirusha mawe na kufanya mizaha, na kuchekwa,

lakini imekomaa sasa. Hiyo ni kweli kabisa. Saa imewadia. Haleluya! Hiyo ni kweli. Hilo ndilo linalonivutia, kuona Kanisa la Mungu likija pamoja sasa. Tumepigwa *huku* nje, na kupigwa *huko* nje, lakini saa inakuja ambapo Mungu atatufunika sisi sote kwa blanketi, ili kutuvuta ndani, kwa maana adui yuko langoni. Haleluya! Naam, bwana. Alisema, na sasa kuhusu watu Wake, Danieli alisema, “Mambo makuu ya siku za mwisho, mambo haya yatakapotimia, jamani, mambo makuu yatafanywa na watu wakati huo, katika siku hiyo.”

75 Nayo saa imewadia sasa ambapo ule mchezo mkuu wa kuigiza, picha ya Mungu iliyowekwa, ya mvua ya vuli. Yoeli alisema, “Katika siku za mwisho, itakuwa kwamba nitawamwagia watu wote Roho Yangu; na wana wenu na binti zenu watatabiri. Juu ya watumishi wangu wanaume na wanawake nitaimwaga Roho Yangu. Nami nitaonyesha ishara katika mbingu juu, na ishara katika nchi chini, na nguzo za moto, na mvuke wa moshi. Itakuwa, kabla haijaja ile siku ya Bwana iliyo kuu na ya kuogofya, kwamba kila atakayeliitia Jina la Bwana ataokolewa.”

76 Yesu alisema humo ndani, “Mambo haya niyafanyayo Mimi, ninyi nanyi mtayafanya, na makubwa kuliko haya, kwa kuwa Mimi naenda kwa Baba Yangu.” Haleluya! Haleluya! Haya ndiyo aliyosema mle ndani, kwenye—kwenye ninii—Neno huko nyuma, kasema, “Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu likae ndani yenu, ombeni mtakalo nanyi mtapewa.”

77 Miaka michache iliyopita, watu hapa walisema, “Ninyi watu huko juu Maskanini ni watakatifu wanaojifingirisha. Ninyi ni *haya* yote, *yale*, na *mengineyo*. Mna kichaa!”

78 Lakini, loo, jamani, tumesimama juu ya Mwamba huo, hiyo ni Kweli, hata ubatizo wa Roho Mtakatifu, na sasa nguvu za Mwenyezi Mungu zimefanyizwa kanisani, zikija. Haleluya! Ninatazamia wakati ambapo Mungu atakitikisa hiki kitu chote, kila mahali. Ndugu, tayari limeanza sasa hivi. Linaendelea. Hiyo ni kweli.

79 Uungu Wake. Yeye ni nani? Baadhi yao humfanya kuwa mtoto mdogo huko nyuma. Yeye Ndiye aliyesimama juu ya yasiyoonekana, loo, jamani, jukwaa, akainyoosha mikono Yake, akanena na kusema, “Iwe nuru,” ikawa nuru. Huyo alikuwa ni Yesu Kristo. “Kwa maana alikuwako ulimwenguni, nao ulimwengu uliumbwa na Yeye, wala ulimwengu haukumtambua.” Alikuwa . . . Yeye ni Uungu wa Mungu. Angalieni aliyofanya kule nyuma. Nena kuhusu ya kimiujiza huko nyuma; unanena kuhusu kupiga kelele? Alipofanya mambo ya kimiujiza, kuviumba vitu vilivyomo sasa, kutokana na vitu visivyokuwepo, alinena na ikawa.

80 Na Nguvu zizo hizo, Kristo yeye yule! Haleluya! Acha watu wa kimsingi, acha hao watu wanaozikana Nguvu za Mungu,

waseme ni uongo, bali Nguvu zizo hizo zilizounena ulimwengu ukawa ziko katika wale watu walio na Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli. Wanaume kwa wanawake, wakati umewadia kwetu kujua wewe ni nani. Ibilisi anajaribu kukuficha, kukwambia ya kwamba wewe ni maskini kitu kidogo kilichodhalilishwa. Sivyo ulivyo. Ninyi ni wana na binti za Mungu. Uungu hauko Mbinguni; uko ndani yenu. Haleluya! Najua mnafikiri nina kichaa, lakini acha nikwambie jambo fulani, ndugu: Unapotambua kwamba Mwenyezi Mungu anaishi ndani yako, Uzima usiopatikana na mauti, "Uzima Wangu natoa, Zoe," Uzima wa Mungu uko ndani ya mwanadamu!

81 Alisimama kule nyuma, Yeye ni Muumba wa vitu vyote. Aliumba uhai; vyura, loo, nyuki, mabata, kuku, wanyama, aliumba kila kitu. "Na hakuna chochote kilichoumbwa ila kile kilichoumbwa na Yeye." Nani? Kristo, Mungu! "Alishusha yale mapigo, na kila kitu katika siku za Misri." Nani? Kristo! "Alivinyamazisha vi—vinywa vya simba. Alizima ukali wa moto. Waliepuka makali ya upanga. Waliwafufua wafu kutoka kaburini." Nani? Kristo! Loo, jamani, itakuwaje! Yeye ni nani? Kristo, Mungu!

82 Na, ndugu, dada, Uungu huo uko ndani yako. "Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena. Lakini ninyi mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari." Kristo katika hori? Hapana. Kristo ndani yako! Haleluya! Hatumwabudu Kristo aliye horini, bali Kristo aliye ndani yako, Roho Mtakatifu, tumaini la Uzima, haleluya, Muumba, Mungu Mwenyewe akiishi ndani ya mwanadamu. "Bado haijaonekana tutakavyokuwa, lakini tutamwona jinsi alivyo." Kwa maana tutafanywa kama Yeye, Roho ndani ya mwanadamu.

83 Hamna nafasi Kwake. Watu karibu hapa wakisema wao—wao ni wa Kristo, kanisa lao ni la Kristo, wanaenda kwa ninii . . . Basi ni nini kilichotukia jana usiku? Walifungua zawadi zao za Krismasi. Hebu tuone kuhusu baba; mle ndani kulikuwa na ninii . . . ilikuwa chini ya mti wa Krismasi, wa watu wengi, jana usiku, liliwekwa sanduku kubwa la bia mahali fulani. Hakuna nafasi kwa ajili ya Yesu; yote ni ya bia. Wakafungua zawadi ya mama, jozi ya karata. Hakuna nafasi kwa ajili ya Kristo; karata. Hiyo ni kweli. Badala ya Biblia ndogo ama kitu fulani kwa ajili ya watoto, ni kitabu kidogo cha G-man, ama maskini kitu kama hicho. Hakuna nafasi kwa ajili ya Yesu. Badala ya kwenda kanisani, wanaenda kwenye sinema, madansi, kila kitu, na kujiita Wakristo.

84 Ndugu, wakati Uungu wa Mungu, kwa njia ya Roho Mtakatifu, unapoingia ndani ya moyo wa mwanadamu, unakemea kila kitu ambacho Kristo hajaumba. Unajua hiyo ni Kweli.

85 Mungu, Kristo, tumaini la Utukufu, ndani yako! Sio kwenye kitanda cha mtoto; ndani yako! Huo ulikuwa ni wakati mmoja, Mungu alikuwa huko nyuma katika mwanzo, ndipo akaingia ndani ya Musa, akaja katika wana wa Israeli, Akaja kwenye kitanda cha mtoto. Lakini sasa watamwabudu huko nyuma kabisa kama kitu fulani cha kabla ya historia; wakati, Kristo yuko ndani yako! Huyu hapa, leo hii, Mwana wa Mungu akipanda juu, Kanisa Lake kuu linasonga mbele.

86 Siku hizi kanisa lina supu za jioni, chakula cha sambusa za jioni, waone ni nani anayeweza kuvaa nadhifu zaidi, wanaingia kanisani kwa fahari, utukufu, ni nani aliye na kanisa bora zaidi, viti bora zaidi, ni nani anayeweza kucheza *hiki,* ni nani anayeweza kufanya *kile.* Wala hakuna nafasi; nyakati zote wana jambo lingine la kufanya kando na maombi. Hawawezi kuomba tena. Wana jambo lingine la kufanya; hawawezi kuomba tena. Kamwe hawawezi kumpenda, kumtumikia Mungu kama walivyokuwa wakifanya. "Hakuna nafasi Kwake katika nyumba ya wageni." Na hii ni katika wakati wa mwisho, ewe rafiki. "Hakuna nafasi Kwake katika nyumba ya wageni." Bila shaka, najua ile nyumba ya wageni ilimaanisha nini, lakini ninarejelea nyumba hii ya wageni.

87 Lakini Biblia ilisema, "Siku hiyo, mlozi utachanua maua, shauku ya mwanadamu itakoma; kwa sababu yeye anaenda kwenye nyumba yake ya milele, nao waombolezao huzunguka mitaani; au kamba ya fedha kukatika, au mtungi kuvunjika kisimani." Loo, rehema, rafiki yangu!

88 Lakini nabii pia alisema, "Itakuwa Nuru wakati wa jioni." Hiyo ni kweli. Njia ya Utukufuni bila shaka mtaipata. Hiyo ni kweli. Wakati wa jioni umefika. Kanisa sasa, ambalo hapo awali lilikuwa limevikwa kama maskini tukio lile la hori ambalo tumepitia, limefikia mahali sasa ambapo watu wanatambua kwamba Uungu na Nguvu za Mwenyezi Mungu zinaishi ndani ya mwanadamu.

89 Loo, ndugu, dada, hebu niseme nanyi, katika Jina la Yesu, asubuhi ya leo. Mngali mnanisikia? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Loo, jamani, hebu niwaambie jambo fulani!

90 Wakati unakuja ambapo wanawake na wanaume karibu wanafanana. Wanavalia sawa kabisa, huwezi kutofautisha mmoja na mwingine. Hiyo ni kweli. Mambo hayo yote katika Biblia, yaliyosemwa yangetimia, yako hapa. Hiyo ni kweli. Unajua hiyo ni Kweli. Je, ni Kweli? Je, ni Kweli? Na ndivyo ilivyo, ni Kweli. Wanatenda sawa, wanafanana, wanatukana sawa, wanazungumza sawa. Biblia ilisema itakuwa hivyo. Yeye alisema, "Katika siku za mwisho, kwamba nyakati za hatari zitakuja. Watu watakuwa wenye kujipenda wenyewe, kuliko kumpenda Mungu; wasiofanya suluhu, wasingiziaji." Je, yamefika? Hiyo ni Kweli.

91 Loo, utukufu kwa Mungu! Ninahisi kitu fulani kikifingirika nafsini mwangu! Jamani, loo, ninapotazama hapa nje! “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Nuhu alikuwa na baadhi ya watu waaminifu siku hizo. Mungu ana watu waaminifu siku hizi. Saa inakuja, mpangilio huu mkuu wa mchezo wa kuigiza.

92 Wanaume kwa wanawake, kama Roho Mtakatifu anakaa ndani yenu, Kristo aliyezaliwa miaka elfu moja na mia tisa iliyopita alifikia utu uzima. Kamwe hakukaa kwenye susu.

93 Na leo hii, huo ukumbusho wa siku ya kuzaliwa Kwake, wao wanafanya nini? Wanatafuta mti fulani, wanaukata, wanatengeneza mti wa Krismasi kwa ajili ya watoto. Lakini wanawazia . . . Hilo ni sawa; silipigi hilo teke. Lakini jambo ni kwamba, wao huushughulikia zaidi mti wa Krismasi kuliko wanavyomshughulikia Kristo.

94 Kris Kringle yuko kote nchini. Alikuwa nani? Mjerumani, mtakatifu wa Kikatoliki miaka mingi iliyopita, mzee aliyeenda huku na huko akitenda mema. Na siku hizi imekuwa karibu ni ibada. Hiyo ni kweli. Ni sawa kuwaambia watoto, ama chochote unachotaka kufanya, nijuavyo mimi. Lakini jambo ni kwamba, ni rahisi sana kuanguka katika utaratibu huo upande mwingine, na kumsukumia Kristo nje, misingi halisi ya Kristo, ya Krismasi. Naye mtu anamchukua Kris Kringle badala ya Krismasi halisi, hiyo ni kweli, “Hakuna nafasi kwa ajili Yake katika nyumba ya wageni.”

95 Yote yameonyeshwa, kama tungekuwa na wakati. Najua muda unaenda, na kunachelewa.

96 Lakini angalieni, marafiki, saa imewadia, na sasa ipo, ambapo mchezo mkuu wa kuigiza wa Mungu umewekwa hapa mbele zetu. Mwana wa Mungu, ambaye alikuwa katika susu, yuko moyoni sasa. Yeye ni Uungu wa Mungu. Yeye ni Mungu, Muumba. Alisema, “Mambo yote . . . Alikuwako ulimwenguni, nao ulimwengu uliumbwa na Yeye, wala ulimwengu haukumtambua.”

97 Basi, siku hizi, hiyo ndiyo shida ya kanisa. Tumaini la Utukufu, ubatizo wa Roho Mtakatifu, umeingia katika mioyo ya watu, wala hawatambui ni nini. Wanafikiri ni kujiunga kidogo na kanisa, ama kitu kama hicho.

98 Lakini huyo ni Mungu, Muumba, akiishi ndani yako, na kukupa Nguvu zote. Na wewe unamiliki chochote alichokuwa nacho. Kwa hiyo Yuko ndani yenu kujiepusha na maovu, kutenda mema, kujiepusha na maovu na kukimbilia haki, kujiepusha na majaribu. Uovu wote, chuki, ugomvi, husuda, na kadhalika, jiepushe nayo, kwa maana hayo yatamwondoa moyoni mwako. Laiti ungalimpokea, kumkumbatia na kumpenda, na kumshika moyoni mwako na kumpenda! Naweza kukwambia, kanisa pamoja katika Nguvu za aina hiyo, lina Nguvu za kuzifunga

mbingu, kuwaponya wagonjwa, kuyafungua macho ya vipofu, haleluya, viziwi kunena . . . mabubu kunena, na viziwi kusikia, viwete kutembea, vipofu kuona. Kwa nini? Ni kutambua Nguvu za Mwenyezi Mungu ndani ya moyo wako. Huyo hapo, ule Uungu.

99 Mnampenda? Si ajabu mshairi alisema:

> Neema ya ajabu! jinsi inavyosikika tamu,
> Iliyomwokoa mwovu kama mimi!
> Wakati mmoja nilikuwa nimepotea, lakini sasa
> nimepatikana,
> Nilikuwa kipofu, bali sasa ninaona.

100 Ndugu mpendwa, dada, kama hujapokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, asubuhi ya leo, kimbia katika Ufalme wa Mungu upesi uwezavyo. Wakati wa kutiwa muhuri unaendelea. Adui ameingia kama mafuriko; Yeye anainua kiwango dhidi yake. Mchezo wa kuigiza umewekwa. Kanisa linaenda nyumbani kwa uhakika tu kama chochote kile. Huna haja ya kungojea sikuzote, rafiki. Huna muda wote wa kungojea. Afadhali uje sasa. Afadhali uje leo, hiyo ni kweli, "wakati leo ni leo." Njoo sasa.

101 Kumbukeni, marafiki, linaweza kuonekana la kigeni. Ulimwengu kamwe . . . Dini ya Kristo kamwe haikuwa maarufu. Sikuzote imekuwa isiyopendwa na watu, njia za Mungu, kwa sababu ibilisi ndiye "mfalme wa uwezo wa anga." Ana serikali zote. Kila serikali inatawaliwa na ibilisi, kulingana na Biblia. Ibilisi alisema ndivyo ilivyo. Hiyo ni kweli. Anaongoza serikali zote.

102 Halafu Biblia ilisema, "Furahini, enyi Malaika wote watakatifu, na ninyi watakatifu juu ya nchi; kwa maana falme za ulimwengu huu zimekuwa falme za Mungu wetu, na za Kristo Wake, nazo . . . Yeye atatawala."

103 Shetani alimpeleka Yesu juu ya mlima, akamwonyesha milki zote za dunia, kasema, "Hizi zote ni zangu, nami nitakupa Wewe."

104 Naye Yesu akasema, "Ondoka hapa, Shetani." Hiyo ni kweli. Hakuwa anajali . . .

105 Alisema, "Kama ufalme Wangu, wa ulimwengu huu, ningeweza kuita majeshi yoyote ya Malaika; lakini Ufalme Wangu si wa ulimwengu huu, bali Ufalme Wangu uko Mbinguni."

106 Naye akasema, "Ufalme wa Mungu utakuwa ndani yenu." Hivyo basi, majeshi na uwezo, na msaada wa Malaika Watakatifu (haleluya) uko ndani yako, asubuhi ya leo, kwa Uungu wa Kristo, kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Naam, bwana.

107 Wewe ni nani, asubuhi ya leo? Kristo Yesu ni nani? Yuko ndani yako kadiri utakavyomruhusu awe. Anasukuma, akijaribu

kuingia ndani yako, kuingia ndani yako leo. Nawe unasimama kando na kustaajabu, na kutazama na kukaza macho, na kujizuia kwa muda kidogo. Usifanye hivyo. Sogea moja kwa moja kwenye kifua cha Mungu. Saa imewadia. Haleluya!

108 Loo, jinsi ninavyompenda! Yeye yuaja moja ya siku hizi. Ninataka kumwona. Nawe je? Ninataka kumwona. Naamini tutamwona. Nawe je? Yuko hapa sasa. Nguvu Zake zinasonga.

109 Ni nini kinachowafanya watu kulia na kupiga makelele, kuendelea? Kuna nini? Ni Roho Mtakatifu akitenda kazi ndani yao. Laiti wangeweza tu kutambua na—na kumkumbatia! Mkumbatie Roho Mtakatifu, mwamini Yeye, mkumbatie kifuani mwako. Ishi maisha mema, usifanye chochote kinachoweza kumzuia. Sema, "Ee Bwana Yesu, nakutaka Wewe. Nataka Wewe usimame karibu nami. Nitasimama karibu Nawe, Baba." Basi unapofanya hivyo, Yeye anasukuma tu apate kuingia ndani yako. Anapataka humo ndani. Anakubembeleza uje Kwake, wakati wote.

110 Sasa, marafiki, ninajua hiyo kuwa ni Kweli. Najua watu hawatambui wewe ni nani. Kila mtu hapa ndani anaweza kuishi juu ya dhambi, anaweza kuishi bila dhambi, kuishi ndani ya Mungu. Utafanya makosa, lakini Damu ya Kristo itakusamehe. "Baba, wasamehe, kwa kuwa hawajui watendalo." Hiyo ni kweli? Nguvu zile zile za Kristo zilizosulubishwa juu ya msalaba wa Kalvari, Mungu yeye yule aliyemfufua katika siku za ule ufufuo, zimo ndani yenu sasa, ninyi mlio na Roho Mtakatifu. Loo, hivi hamumpendi? Loo, jamani! Isikie Sauti Yake ikiita leo.

111 Msogeze kwenye kifua chako cha karibu, na useme, ama karibu kifuani mwako, na useme, "Sasa, Bwana Yesu, nimekuwa tofauti kidogo, kuanzia siku hii ya Krismasi ninatambua Wewe ni Nani sasa. Wakati mmoja nilikuabudu kama mtoto mchanga horini. Nilikuona huko nyuma kama maskini jamaa mdogo, miaka elfu moja mia tisa iliyopita, nami nikawazia, 'Loo, laiti ningaliweza kwenda Yerusalemu!'"

112 Siku hizi, wanapata pasi na kila kitu, kuenda huko kwenye—kwenye susu, mpaka mahali alipozaliwa, hori lile lile. Lakini, marafiki, si *kule* juu alikozaliwa; ni papa *hapa* alipozaliwa. Mungu amemshusha kwa kila mmoja wetu, na Utu Wake ulio hai unaishi ndani yetu. Loo, Muumba, yule aliyeumba ulimwengu, na kuumba mbingu, akaumba dunia, akaumba mwanadamu, yuko moja kwa moja ndani ya kila mtu binafsi aliye na ubatizo wa Roho Mtakatifu leo hii. Jambo ndilo hilo, hiyo ndiyo siri, mpokee Roho Mtakatifu. Yuko ndani yako. Yeye ndiye tumaini la Utukufu.

113 Pia angalia hapa, katika Agano la Kale, kama nilivyolirejea mara nyingi, wakati mkataba ulipofanywa, ulipasuliwa, juu ya maiti ya mnyama aliyekufa. Na hiyo mikataba miwili

ilibidi iunganishwe, mkataba huo ilibidi kuumana mmoja na mwingine.

114 Na, leo, Mungu amefanya mkataba. Si kwa sababu ulikuwa mwema, si kwa sababu ulikuwa umejiunga na kanisa, si kwa sababu ulikuwa na hadhi nzuri katika jamii. Unaweza ukawa mzuri sana, unaweza ukaishi maisha safi, unaweza kwenda kanisani kila siku, unaweza kutoa sadaka kila siku, unaweza kutoa sehemu ya pesa zako, unaweza kuacha dhambi zote za ulimwengu, na kila kitu, na uishi mkweli na mwaminifu tu uwezavyo, nawe utaikosa Mbingu kama vile Mashariki ilivyo mbali na Magharibi. Hiyo ni kweli. Hatuokolewi kwa wema, lakini tunanunuliwa kwa rehema Zake, kwamba Mungu alitaka kuwafanya wana na binti. Wema kamwe hauwafanyi. Roho wa Mungu huwafanya. Kama haikuwa hivyo, isingalimlazimu kumtuma Roho Mtakatifu.

115 Roho Mtakatifu angewezaje kuwa mkamilifu isipo-. . . mkataba u—ungewezaje kukamilika? Yesu alisema, "Nitaenda, lakini nitakuja tena; na niwe pamoja nanyi, hata ndani yenu. Ombeni Baba, Naye atawapa Roho Mtakatifu. Atakaa nanyi, milele."

116 Nao watu wanaweka majina yao kwenye vitabu vya kanisa, wanajaribu kufungua ukurasa mpya siku ya Krismasi, wanajaribu kwenda kule kanisani na kutoa sifa chache kwa hori huko nyuma. Wakati, Roho Mtakatifu akisukumiza kila mahali, akijaribu kutafuta . . . Nao ulimwengu umewafanya vipofu sana hivi kwamba wangetembea huko na kusema, "Vema, hilo ni kundi la watakatifu wanaojifingirisha." Kama tu ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo ilivyo sasa.

117 Kuja kwa Mwana wa Mungu kumekaribia! Hiyo ni kweli. Na ni wale tu waliotiwa nguvu na Roho Mtakatifu, ambao wana Uzima usiopatikana na mauti ukiishi ndani yao, Roho Mtakatifu, hao ndio wale watakaovutwa kutoka hapa, hakika tu kama chochote kile.

118 Kulikuwa na kitu kingine kuhusu safina hiyo ndogo ya kale, katika siku za Nuhu, kilichokuwa kikielea juu ya maji. Kilikuwa kikivuta nguvu kutoka Juu. Kulikuwako na nuru juu yake, kwamba Utukufu wa Mungu unang'aa kutoka Mbinguni, ukashuka juu ya kile chumba cha juu.

119 Nami nawaambia, leo, marafiki, sikieni neno langu. Kuna Nguvu zinazovuta, si kutoka kanisani, si kutoka kwa mchungaji, bali kutoka Utukufuni, ubatizo wa Roho Mtakatifu ukishuka katika mkondo huo wa kweli, kulivuta Kanisa! Ni kitu gani? Nguvu za Mungu, kuufikia Uzima Wake, *Zoe*.

120 "Mambo haya niyafanyayo ninyi nanyi mtayafanya; makubwa kuliko haya mtayafanya." Aliteswa, alichekwa, alidhihakiwa, kisha akafa, na kuingia kaburini. Lakini Yeye alikuwa mkweli, alikuwa na Roho wa Mungu ndani Yake,

naye Mungu akamfufua. Tukienda kwa njia ile ile, pia sisi tutafufuliwa. Loo, haleluya! Nampenda!

121 Bado mnanisikia? Mnampenda? Unampenda kwa moyo wako wote? Yeye si ni wa ajabu? Loo, jamani!

> Jicho limeona, sikio limesikia, yaliyoandikwa
> katika Neno la Mungu;
> Yeye si ni wa ajabu, wa ajabu?

Na tuinamishe vichwa vyetu.

122 Baba wa Mbinguni, Ee Yesu, ninaitazamia saa moja kuu. Ninaiona ikija. Naona hakuna matumaini popote pengine. Ninaona wakati ukisonga mbele. Ninaona zile taa kuu nyekundu, za ukomunisti, zikiyumbayumba kote duniani. Ninaona makanisa ya kawaida yakiinua bendera dhidi ya Kanisa Lako, wakijaribu kuwahukumu, yakisema, "Uponyaji wa Kiungu ni makosa. Ni lundo la ulokole." Mswada katika Ikulu yetu wenyewe, wa kulifunga.

123 Loo, lakini, Mungu, hivi majuzi, nikiwa nimeketi pale na kuwaona hao watu watakatifu, wote wameangazwa kwa Nguvu za Mungu, nikiziangalia nyuso zao na kuuona utukufu wa Mungu! Wanaweza kuwa kama wale wana wa Kiebrania kwenye ile tanuru ya moto. "Kamwe hatutaanguka chini. Hapana. Mungu wetu anaweza kutukomboa. Utakuja upesi, Bwana Yesu."

124 Nami naona saa inaingia, wakati, "Mfano wa utauwa walio nao watu, lakini wanakana Nguvu zake; hao nao mjiepushe nao," Wewe ulisema, Roho akinena kwa ajili ya siku za mwisho. Nasi hapa katika siku hiyo, leo.

125 Hili hapa kanisa letu dogo limeketi hapa, Bwana, wanaume na wanawake ambao ninaamini wanakupenda. Nami naomba, Mungu, kwamba huyo Roho ambaye amejaza wingi wa mioyo yao, siku zilizopita, sasa atakuja kwa kilindi zaidi, zaidi. Jalia waweke kando kila uovu, kila ugomvi, kila kitu ambacho hakifanani na Wewe, na wapande juu leo hii. Si kwa hori, bali Kalvari. Sio Kalvari kwa jumla, bali kwa Kristo, tumaini la Utukufu, Uungu wa Mungu, ukuu wa Mungu, Nguvu za Mungu ambazo sasa zimo mioyoni mwetu, zikijaribu kutuvuta kutoka kwenye mambo ya ulimwengu, ili apate kututoa katika dunia hii siku moja, kutupeleka kwenye Nchi iliyo bora zaidi. Mungu, tujalie leo. Sikia maombi ya mtumishi Wako, na uzungumze na hawa watu.

126 Kama kuna yeyote aliyepotea, humu ndani, yeyote asiye na Roho Mtakatifu, jalia wapokee kutoka Kwako, asubuhi ya leo. Tujalie, Mungu mpendwa, kwa maana tunaomba katika Jina la Mwanao mpendwa, Yesu; Ambaye miaka elfu moja mia tisa iliyopita alizaliwa horini, Ambaye aliteseka miaka thelathini na mitatu baadaye pale Kalvari, kwa ajili ya dhambi zetu, Ambaye alipaa Juu, siku chache baada ya hapo, siku arobaini baadaye.

Alipokelewa juu Utukufuni, kisha siku kumi baadaye akaja tena katika Nguvu za Roho Mtakatifu, na sasa anaishi Kanisani. Na hivi karibuni, kwa Nguvu zile zile zilizomfufua, Roho Mtakatifu Kanisani, kuliondoa. Ee Mungu, njoo, sivyo, na kuliokoa Kanisa? Kwa kuwa tunaomba katika Jina Lake.

127 Huku umeinamisha kichwa chako, tutaimba, *Anaita Leo*. Ikiwa kuna mtu yeyote hapa asiye na Kristo, asiye na Mungu, asiye na tumaini, waweza kuja sasa?

> Anaita leo, anaita leo,
> Yesu anaita, Anaita kwa upendo leo.
>
> Yesu anaita kwa upole leo,
> Anaita leo . . .

128 Je, huna Mungu, huna tumaini, huna Kristo? Je, mnatambua, enyi Wakristo, kwamba hamna uzima kamili wa Neno la Mungu? Hivi hamtakuja?

> . . . mbali zaidi?
>
> Anaita, anaita leo, anaita leo,
> Yesu anaita leo, anaita kwa upole leo.

129 Sikiliza, Baba yuko hapa na Yeye—Yeye anataka kukuokoa, ikiwa hujaokolewa. Sikujui. Lakini, sikilizeni, marafiki, ninataka kuwafanyia jambo fulani asubuhi ya leo, mkiwa mmesimama hapa. Nawatakeni myafumbe tu macho yenu. Ninataka kushusha pazia hapa na kuwaruhusu mtazame mahali fulani. Tutafanya matembezi kidogo, asubuhi ya leo, sasa wakati anapoupiga wimbo huo. Nitashusha pazia, kwa ajili ya wale tu wanaoketi katika Maskani hii, vijana kwa wazee, na wote.

130 Nitaangalia kwenye malango ya Kuzimu, kwa muda kidogo, asubuhi ya leo. Wanajua kule chini ni wakati wa Krismasi huku juu. Wanajua walichofanya wakati wa Krismasi. Baadhi yao wamekunywa pombe, wengine wao wametangatanga, wengine walikuwa kanisani, wengine walidhihaki, wengine walifanya mizaha. Vipi kama gofu hili la mtu linalotambaa lingeweza kurudi hapa kwenye mlango huu wa kanisa asubuhi ya leo? Unajua, Krismasi ijayo huenda ukawa huko. Huenda utakuwa umekuwa huko kwa mwaka mmoja, Krismasi ijayo. Lakini, kumbuka, unashughulika na nafsi za wanadamu; unashughulika na mambo ya kiroho, na kila mmoja wenu hana budi kujibu Siku ya Hukumu. Naweza tu kuwa mkweli. Ninaweza tu kusema, ikiwa hujampokea huyo Kristo asubuhi ya leo, anasimama kwenye mlango ulio wazi! Je, unamtendea vibaya?

131 Nanyi mlio na Roho Mtakatifu, kumbukeni, mtahukumiwa kwa yale mliyofanya Nalo. Huenda umempokea Kristo, kwa Roho Mtakatifu, lakini utahukumiwa; kila mtu anahukumiwa kulingana na kazi alizofanya katika mwili wake. Ukiisha kumpokea Roho Mtakatifu, umefanya nini Naye? Je, umemsengenya jirani yako? Je, umefanya mambo vibaya?

Ikiwa umefanya, kumbuka, ningeanza maisha upya sasa hivi. Niseme, "Bwana Yesu, leo, tangu sasa na kuendelea, nitakuwa kile unachotaka niwe. Ninatambua ni sehemu ya Mungu isiyopatikana na mauti, naye Roho wa Mungu anaishi ndani ya mwili wangu. Na kama mimi—kama nimekosea, Wewe nisamehe sasa. Na—nataka kuja nyumbani. Na—nataka kuwa bora zaidi."

132 Mthibitishe humo ndani, asubuhi ya leo, namna hiyo tu. Inua tu mkono wako, kwa ajili yangu, huko nyuma. Useme, "Ninataka kuanza upya leo, Ndugu Branham." Nimeinua mkono wangu, pia; nitaanza upya. Ninataka kumfanyia mengi zaidi kuliko nilivyowahi kufanya! Hivi wewe . . .?. . .

133 Moja ya hadithi za kusikitisha sana nilizowahi kusikia, wakati mmoja. Msichana mmoja, yeye, msichana mrembo sana. Alikuwa katika nyumba nzuri; walimzungumzia habari za Kristo. Ba—baba yake akasema, "Ni—ninamwonea aibu, kasisi." Kwa jamii: atakutana na tabaka hilo la watu kwa sababu yeye ni . . . Sasa, kumbukeni, kama jamii, unajipachika kwenye kitu kinachoitwa "kichaa." Lakini alipata elimu bora sana. Alipojitayarisha kupenya, kuambatana na jamii, na kwenda na tabaka lingine zuri la wanaume, mauti yalimpiga na kitu fulani: alipata mshtuko wa moyo. Mafunzo yake yote hayakumfaa kitu. Alikwenda mahali pengine.

134 Unaelekea wapi asubuhi ya leo? Unaotea nini? Sijali ni kundi la aina gani, kila mmoja wenu, utaingia katika Umilele moja ya siku hizi. Na bila Kristo, bila Roho Mtakatifu, nafsi yako imepotea. Kumbuka hilo.

135 Huwezi kukutana na hilo ila tu kwa kumkubali Kristo, kwa Roho Mtakatifu. Ikiwa Yeye yuko ndani yako, Yeye ni Nguvu za Mungu. Ishi Kwazo. Yeye ni Mungu ndani yako. Biblia ilisema, "Mnakuwa miungu." Hiyo ni kweli. "Je, ninyi nyote si miungu?" Naye Yesu alisema . . .

Mafarisayo pale, walisema, "Unajifanya Mungu."

Kasema, "Je, haikuandikwa katika torati yenu kwamba, 'nyinyi ni miungu'?"

Alimfanya Musa kuwa mungu kwa Farao.

136 Naye akakufanya wewe mungu kwa watu. Hiyo ni kweli. Nanyi, asubuhi ya leo, ni nyaraka zilizoandikwa za Mungu. Maisha ye—yenu ni ya Mungu, na hata humbeba huyo Roho Mtakatifu.

137 Angalieni hapa, marafiki, msiliache hili liwapite. Kamwe usiache jambo hili likupite kama jambo dogo la uwongo! . . .?. . .

138 Baba, tunakuja asubuhi ya leo, kama watoto Wako wanyenyekevu. Ninatambua kwamba—kwamba tunaishi katika ile saa ya mwisho, wakati wa kufunga, jambo fulani linaweza kutukia wakati wowote. Wanaume, wanawake, wavulana, au wasichana, hapa, wasio na Mungu. Nami nakuomba Wewe,

Baba, uturehemu. Ninakuomba Wewe, uwarehemu wale waliopokea, na wasitambue kwamba Wewe uko karibu, mioyoni mwao. Na kutambua kwamba mambo madogo ya ulimwenguni, kwa njia ya matunzo, yanafifia. Ninaomba, Mungu, ya kwamba kila mtu hapa asubuhi ya leo atawekwa wakfu Kwako kabisa, kwa ajili ya siku zijazo, na bila kujali tutangoja kwa muda gani zaidi kabla ya Kuja Kwako. Tunaamini kumekaribia sana sasa.

139 Na baada ya muda, watu watajaribu kuokolewa; hawawezi. Ninawazia juu ya wale vijana usiku ule, kule chini madhabahuni, wakijaribu kuokolewa, lakini walikuwa wamevuka mpaka. Hakuna ukombozi kwao; walikuwa wamekwisha, wasingeweza kuokolewa.

140 Baba, na—naomba tu ya kwamba utawabariki, kila mmoja, wakati tungali na wakati, Baba, kwamba watampokea leo. Kwa kuwa tunaomba katika Yesu Kristo. Amina.

141 Hebu tusimame. Ni wangapi wanaompenda kwa moyo wenu wote? Je, hutaki kumkaribia Yeye kidogo tu, kumpenda Yeye zaidi kidogo tu? Hebu tuimbe *Natoa Yote*, tunapomwinulia mikono yetu, asubuhi ya leo, . . .?. . .Je, mtafanya hivyo? Tupe mwongozo hapo kwake, dada.

> Natoa, (natoa yote!) (Tabia zako zote, njia zako zote.)
> . . . toa, (natoa yote!)
> Yote Kwako, Mwokozi wangu mbarikiwa,
> Natoa yote.

Kweli unalimaanisha?

> Natoa, (natoa yote!)
> Natoa, (natoa yote!)
> Yote Kwako, Mwokozi wangu mbarikiwa,
> Natoa yote.

142 Ee Baba, uturehemu. Tunakupenda, sana, Bwana. Baadhi ya siku hizi parapanda italia. Ninaweza nikawa huko nje hudumani mahali fulani. Bwana, nitakuwa nikifikiria kuhusu kanisa basi. Pepo zinapoanza kuvuma, ulimwengu utakapoanza kutikisika. Wengine wanasema, "Kuna nini?" Anga zinageuka kuwa nyekundu, saa ya hukumu imekaribia. Nitawazia, "Loo, yuko wapi Ndugu Graham? Yuko wapi . . . Loo, wako nyumbani." Lakini, Baba, basi, baada ya kitambo kidogo, tutasikia sauti isiyopata kusikika hapo awali, ile Baragumu; Malaika anapiga Baragumu. Ee Mungu, wale walioingia kwenye chumba cha mauti, watafufuka. Jinsi mayowe yatakavyotolewa, "Je, dunia ina shida gani? Hatuwezi kusimama kimya. Nayo inatikisika." Ndipo basi tutanyakuliwa pamoja ili kumlaki hewani.

143 Ee Baba, kama mauti yatatujia kabla ya wakati huo, ninamaanisha kifo cha kawaida cha utengano wa dunia hii hapa, jalia tuingie vyumbani, tukiwa na imani thabiti, tukiwa tumevikwa vazi la Kristo, Roho Mtakatifu. Siku moja hatuna

budi kushuka kule chini, Baba. Nami natambua sina budi kutembea kwenye mstari huo, pia. Uko pale nje mbele yangu mahali fulani, saa hiyo nitakayoingia kwenye chumba hicho cha mauti. Ninaposikia hukumu yangu ikisomwa, sitaki kwenda kama mwoga. Ninataka kwenda kama Wewe ulivyoenda, Bwana. Sio kujaribu kujizungushia vazi langu mwenyewe; lakini kuvikwa vazi la Kristo, Roho Mtakatifu, kama Paulo alivyofanya, na kusema, "Mauti, u wapi uchungu wako? Kaburi, u wapi ushindi wako?" Niingie katika chumba kile chenye giza miongoni mwa wale waliokufa; nikisikiliza basi sauti Yake, ya Malaika Mkuu atakayetoa sauti, nasi tutaitwa kutoka miongoni mwa wafu, kukutana na wapendwa wetu tena.

144 Ee Bwana, tukikosa hayo maishani, maisha yamekuwa si kitu kwetu; tulishindwa. Lakini tukimpata Yeye aliye wa thamani mioyoni mwetu, basi tulipata kusudi lote la Mungu.

145 Loo, jinsi tunavyompenda, asubuhi ya leo! Jalia kila Mkristo, asubuhi ya leo, alione ono hilo upesi, Bwana. Saa inazidi kuchelewa sasa, nami ninaomba ya kwamba Wewe utawaruhusu kuona lile ono na kuushika Uzima, leo, na kuishi milele, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

146 Mnapendana? Geukeni na kupeana mikono ninyi kwa ninyi, mseme, "Mungu akubariki. Kristo awe pamoja nawe." Badala ya "Krismasi Njema," mseme, "Kristo awe pamoja nawe," mnapogeuka. Sasa usiondoke, ge—geuka tu, useme, "Kristo awe nawe." (Kristo awe nawe.)

> Yote . . .

Sasa hebu kidogo.

> Yote Kwako, Mwokozi wangu mbarikiwa,
> Natoa yote.

147 Mbona, nilifikiri ilikuwa baada ya saa sita. Ni baada ya tano, nami nilifikiri ilikuwa ni dakika ishirini baada ya saa sita. Ninii tu . . . [Dada mmoja anasema, "Acha tukae saa nyingine moja."—Mh.] Wasema nini? Amina.

148 Kila mtu anampenda Bwana? Semeni, "Bwana asifiwe." [Kusanyiko linasema, "Bwana asifiwe."—Mh.] Hebu tuseme tu ma—machache, machache tu, si zaidi—si zaidi ya maneno matatu au manne ya ushuhuda, kama, "Nampenda Yesu." Semeni tu, naam, sio zaidi ya hayo. [Mtu fulani anasema, "Nampenda Yesu."] Hiyo ni kweli. Mtu mwingine. ["Nampenda Yesu."] Nampenda! Nampenda! Loo, . . .

> Yesu, Mwokozi, niongoze
> Juu ya bahari yenye dhoruba ya maisha;
> Mawimbi yasiyojulikana mbele yangu yanatanda . . .? . . .

*UUNGU WA YESU KRISTO* SWA49-1225
(The Deity Of Jesus Christ)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza kwenye Siku ya Krismasi, Jumapili asubuhi, tarehe 25 Desemba, 1949, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.


Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:


VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org